



Pearson  
Edexcel

## Mark Scheme (Results)

November 2020

Pearson Edexcel International GCSE  
In Swahili (4SW0)  
Paper 02: Listening

## **Edexcel and BTEC Qualifications**

Edexcel and BTEC qualifications are awarded by Pearson, the UK's largest awarding body. We provide a wide range of qualifications including academic, vocational, occupational and specific programmes for employers. For further information visit our qualifications websites at [www.edexcel.com](http://www.edexcel.com) or [www.btec.co.uk](http://www.btec.co.uk). Alternatively, you can get in touch with us using the details on our contact us page at [www.edexcel.com/contactus](http://www.edexcel.com/contactus).

## **Pearson: helping people progress, everywhere**

Pearson aspires to be the world's leading learning company. Our aim is to help everyone progress in their lives through education. We believe in every kind of learning, for all kinds of people, wherever they are in the world. We've been involved in education for over 150 years, and by working across 70 countries, in 100 languages, we have built an international reputation for our commitment to high standards and raising achievement through innovation in education. Find out more about how we can help you and your students at: [www.pearson.com/uk](http://www.pearson.com/uk)

Autumn 2020

Publications Code 4SW1\_02\_2011\_MS

All the material in this publication is copyright

© Pearson Education Ltd 2020

## General Marking Guidance

- All candidates must receive the same treatment. Examiners must mark the first candidate in exactly the same way as they mark the last.
- Mark schemes should be applied positively. Candidates must be rewarded for what they have shown they can do rather than penalised for omissions.
- Examiners should mark according to the mark scheme not according to their perception of where the grade boundaries may lie.
- There is no ceiling on achievement. All marks on the mark scheme should be used appropriately.
- All the marks on the mark scheme are designed to be awarded. Examiners should always award full marks if deserved, i.e. if the answer matches the mark scheme. Examiners should also be prepared to award zero marks if the candidate's response is not worthy of credit according to the mark scheme.
- Where some judgement is required, mark schemes will provide the principles by which marks will be awarded and exemplification may be limited.
- When examiners are in doubt regarding the application of the mark scheme to a candidate's response, the team leader must be consulted.
- Crossed out work should be marked UNLESS the candidate has replaced it with an alternative response.

Paper 2: Listening mark scheme

Question number	Answer	Mark
1(a)	F	(1)
1(b)	H	(1)
1(c)	G	(1)
1(d)	C	(1)

Question number	Answer	Mark
	B, E	(2)
	A, G	(2)
	C, F	(2)

Question number	Answer	Mark
3(a)	Mombasa	(1)
3(b)	wazazi	(1)
3(c)	ndege	(1)
3(d)	saa moja	(1)
3(e)	kuogelea	(1)
3 (f)	kutembea	

Question number	Answer	Mark
4(a)	(a) Lola - Chanya (+)	(1)
4(b)	(b) Mkude - Chanya na Hasi (+ &-)	(1)
4(c)	(c) Asha - Hasi (-)	(1)
4(d)	(d) Chege - Chanya na Hasi (+ &-)	(1)
4(e)	(e) Abushiri - Chanya na Hasi (+ &-)	(1)
4(f)	(f) Jackson- Hasi (-)	(1)

Question number	Answer	Mark
5(a)	D	(1)
5(b)	B	(1)
5(c)	C	(1)
5(d)	D	(1)
5(e)	A	(1)
5(f)	B	(1)

Question number	Answer	Mark
6(a)	E	(1)
6(b)	L	(1)
6(c)	F	(1)
6(d)	B	(1)
6(e)	I	(1)
6(f)	K	(1)

Question number	Answer	Accept	Reject	Mark
7(a)	hufaa kwa afya			(1)
7(b)	za madukani zina sukari sana	si nzuri kwa afya		(1)
7(c)	ladha	inachangamsha		(1)
7(d)	ghali			(1)
7(e)	hunukia			(1)
7(f)	chungu			(1)

## Transcript

### Usafiri

#### Question 1

##### Example

F1 Ninapoenda mjini, mimi hupanda basi la mwendo kasi.

##### Question 1 Part (a)

M1 Gari moshi kutoka Nairobi hadi Mombasa husafiri polepole.

##### Question 1 Part (b)

F1 Tulipoenda Tumbatu, tulipanda meli na kuona samaki baharini.

##### Question 1 Part (c)

M1 Babu yangu hapendi sana ndege, sijui kwa nini.

##### Question 1 Part (d)

F1 Unaionaje pikipiki yangu mpya?

### Kazi za Nyumbani

#### Question 2

##### Mfano

M1 Ni muhimu kusaidia kufanya kazi za nyumbani. Je, Juma, wewe hufanya kazi gani?

M2 Mimi huosha gari la baba yangu kila jumamosi.

##### Questions

M2 Na wewe je Michael? Unawasaidiaje wazazi nyumbani?

M1 Tangu nilipokuwa mtoto nimekuwa na kazi ya kufagia uwanja wote na kuhakikisha hakuna takataka zozote kwenye uwanja. Pia huwasaidia wazazi wangu kufua nguo zote. Ni kazi ngumu lakini lazima ifanywe.

M2 Na wewe je Lulu?

F1 Mimi ninapenda sana mapishi. Kila jumapili wageni wengi hututembelea nyumbani kwetu. Mimi huanza kupika asubuhi na mapema na wakati wote huhakikisha kwamba vyombo vyote ninavyovitumia vimeoshwa ninapomaliza kupika.

M2 Hatimaye, Omari!

M1 Kila jumamosi mimi hutandika vitanda ingawa kazi niipendayo hasa ni kupiga deki. Ninapenda kumwaga maji sakafuni na kutumia sabuni nyingi sana.

## Likizo

### Question 3

- M2** Ninaitwa Amin. Wakati wa likizo wazazi wangu walitaka tuende New York lakini ilikuwa ghali sana kwa hivyo tukaenda kupumzika Mombasa. Ingawa dada yangu mkubwa husafiri na sisi wakati wote, mwaka huu yeye alibaki nyumbani peke yake.

Tulipokuwa uwanja wa ndege tulisubiri takribani masaa matano kabla ya ndege kuruka. Watu wengi walilalamika sana. Safari yenyewe ilichukua saa moja tu. Kwa kweli tulishukuru sana kufika hotelini kwetu baada ya safari hiyo. Mimi nilikwenda kuogelea moja kwa moja kwani ninavutiwa sana na zoezi hilo. Wazazi wangu waliamua kwenda kupumzika chumbani. Wakati wa likizo wao hawapendelei kujishughulisha sana kwa hivyo siku iliyofuata walienda kutembea tu. Sote tulistarehe sana na kujipumzisha vizuri.

## Kuenda Madukani

### Question 4

#### Example

- M1** Ninaitwa Mwamedu. Ninapenda kuenda madukani lakini si wakati wa wikiendi.

#### Question 4a

- F1** Mimi ni Lola. Maduka yananivutia sana. Ninaweza kuenda madukani wakati wowote.

#### Question 4b

- M2** Ninaitwa Mkude. Bei za vitu ni ghali mno madukani ingawa ninastarehe ninapoenda kununua mahitaji yangu.

#### Question 4c

- F1** Jina langu ni Asha. Kwa mawazo yangu kuenda madukani ni upotezaji wa muda. Binadamu anaweza kufanya mengine mengi wakati huo.

#### Question 4d

- M1** Mimi ninaitwa Chege. Kuenda madukani ni raha pale unapoenda pamoja na marafiki zako tu, si pekee.

#### Question 4e

- M2** Mimi ni Abushiri. Kwa kweli ninavutiwa na maduka kwa sababu ninapenda kujinunulia vitu vizuri ingawa umati wa watu hunikera.

#### Question 4f

- M1** Mimi ni Jackson. Maduka makubwa huchosha, kwa hivyo mimi hulazimika kununua vitu kwenye vigenge.

## Mipango

### Question 5

#### Example

M1 Sina mpango maalumu baada ya kumaliza shule.

#### Question 5a

M1 Ninapenda sana kucheza michezo ya video ingawa mama yangu anafikiri ninapoteza muda. Nimemfahamisha kwamba kuna kazi nyingi kwenye sekta ya michezo lakini haelewi.

#### Question 5b

M1 Kwa vile ninafaulu vizuri, mama yangu anataka niwe wakili. Anasema nitaweza kukutana na watu wengi na kuitetea jamii yangu.

#### Question 5c

M1 Ninapenda kukutana na watu, lakini ni mshahara mzuri unaonivutia zaidi. Ninataka kuwa na uwezo wa kuishi maisha yenye starehe.

#### Question 5d

M1 Nilipomsaidia mama dukani kwake, niliweza kuona faida ya kujijaji. Inabidi kufanya kazi sana lakini unajitegemea. Nilipolifanyia kazi shirika moja la kujitolea, sikufurahia kabisa kufuata maelekezo ya mkuu wangu.

#### Question 5e

M1 Kuna wakati nilikuwa na uhakika wa kazi ambayo ningependa kufanya ukubwani. Nilipowaona marubani wa ndege na sare zao, nilipata hamu kubwa ya kufanya kazi yao.

#### Question 5f

M1 Lakini kwa sasa bado mipango yangu haijakamilika. Mama ana shauku ya kuniona nikitimiza mipango yangu na kufaulu maishani.



## Ulinzi wa Mazingira

### Question 6

- M1** Aaliyah, wewe hufanya nini ili kuhifadhi mazingira?  
**F1** Mimi huenda shuleni kwa baiskeli yangu. Sipandi gari wala basi kwani sitaki kujihusisha na shughuli zinazoongeza moshi mchafu na kuharibu mazingira. Inabidi niwe mwangalifu sana ninapoendesha baiskeli kwenye barabara kuu kwani madereva wengi huwa na haraka na hawawajali waendesha baiskeli.
- M1** Wewe je Raymond?  
**M2** Mimi ninafikiri inabidi watu wafanye vitu vidogo vidogo ili kulinda mazingira. Binafsi situmii mifuko ya plastiki kwani rais wetu alipiga marufuku matumizi yake na mimi ninafuata sheria. Lakini pia mimi huoga kwa kutumia ndoo kwa hivyo hutumia maji kidogo sana.
- M2** Tuambie Zaidani, wewe una mawazo gani kuhusu kuhifadhi mazingira  
**M1** Mimi ninaongoza kikundi cha vijana ambao hukutana kila mwezi kusafisha fukwe zetu. Watu hutupa taka hovyoy kabisa mchangani. Juzi tulikuta chupa, vikombe vya plastiki na mirija. Itabidi serikali ichukue hatua dhidi ya kutupa taka ufukweni.

## Vinywaji

### Question 7

- F1** Je George, unapenda kunywa nini siku za joto?  
**M1** Mimi ninapenda sana kunywa soda baridi kwa sababu huwa tamu sana. Ninafahamu kwamba soda huwa na sukari nyingi ambayo si nzuri kwa meno.
- F1** Ni kweli. Je, hunywi vinywaji vingine?  
**M1** Ninapoamka asubuhi hunywa juisi ya matunda, tena hununua matunda yangu mwenyewe. Ninapenda hasa machungwa na huyakamua mwenyewe. Hivyo basi hupata kinywaji ambacho kinafaa kwa afya yangu. Nimegundua kwamba juisi za matunda kutoka madukani zimejazwa sukari kupita kiasi na ni mbaya kwa afya zetu kwa hivyo sizinywi.
- F1** Je, wewe hunywa vinywaji vyovyote vya moto?  
**M1** Ndiyo, ili kuwa na siku nzuri, mimi hunywa kinywaji cha moto kila asubuhi. Ladha ya chai tamu ya maziwa hunichangamsha. Ni tofauti na chaguo la baba yangu ambaye hunywa chai kavu. Sisi huagizia chai yetu moja kwa moja kutoka kwa wakulima ingawa ni ghali zaidi na hutugarimu pesa nyingi, lakini huwa na ladha ambayo haipatikani popote kwengine duniani.
- F1** Kmbe! Nyinyi hunywa kahawa nyumbani?  
**M1** Mama yangu ni mpenzi wa kahawa. Yeye hunywa vikombe vitatu kila siku. Hununua kahawa zilizosagwa kwenye kinu kwani zinanukia zaidi. Anapoichemsha sote hufurahia harufu yake. Nimejaribu kunywa kahawa mara nyingi lakini kwangu mimi ni chungu. Sijui mama yangu anainywaje!
- F1** Basi siku njema.  
**M1** Asante. Na wewe pia.

Pearson Education Limited. Registered company number 872828  
with its registered office at 80 Strand, London, WC2R 0RL, United Kingdom